**Double Up Food Bucks na Produce Match**
**Uthibitishaji wa Wauzaji Wanaostahiki**
UTHIBITISHAJI ULIOWEKWA SAINI LAZIMA UWE UMEREKOD
KABLA YA KUREJESHWA KWA FEDHA

-Utatumika kuanzia Januari 1, 2026 – Desemba 31, 2026-

**Jina la Soko:** ______________________________________________________

**Jina la Biashara ya Muuzaji:** ______________________________________________________

**Anwani**:_______________________________________ **Jiji:**___________________ **Jimbo:**_______ **Msimbo wa Eneo:**____________

**Simu:** ____________________ **Barua pepe:** ________________________________________

Uthibitisho huu ni kwa madhumuni ya kumuidhinisha Muuzaji aliyetajwa hapa juu kukubali Double Up Food Bucks (DUFB) na SNAP Cash Produce Match katika soko lililobainishwa (hapa juu) kutoka kwa washiriki wa SNAP na kubadilishana na matunda na mboga zinazostahiki pekee.

- **INATUMIKA KWA**: aina yoyote ya matunda na mboga mbichi, zilizokaushwa au zilizogandishwa <u>bila sukari, mafuta, mawese au chumvi iliyoongezwa.</u> Inajumuisha uyoga, mimea mbichi, maharagwe yaliyokaushwa, na mimea inayoliwa.
- **HAITUMIKI KWA**: njugu, nafaka, nyama, mayai, jibini, bidhaa zilizookwa, vyakula vilivyotayarishwa, vyakula vilivyochachushwa, salsa, kachumbari, jamu, jeli, asali, sida, juisi, chai, au vyakula vingine ambavyo haviendani na miongozo iliyo hapa juu; vitu visivyo vya chakula.

**<u>SOKO LIMEKUBALI:</u>**

1. Kukusanya kutoka kwa Muuzaji Double Up Food Bucks zilizokombolewa na kukokotoa na kumlipa Muuzaji kwa Bucks zozote zilizopokelewa kufikia siku ya mwisho ya msimu wa 2026 wa soko hili.
2. Kufuatilia uuzaji ili kuhakikisha miongozo ya mpango inafuatwa.

**<u>KWA KUTIA SAINI UTHIBITISHAJI HUU, MUUZAJI ANAKUBALI:</u>**

1. Kuwasilisha matunda na mboga zinazostahiki pekee kwa kubadilishana na Double Up Food Bucks na Produce Match.

2. Kutorejesha chenji ya pesa taslimu baada ya ununuzi unaofanywa kwa Double Up Food Bucks au Produce Match.
3. Kutorejesha chenji ya pesa taslimu au mkopo baada ya ununuzi unaofanywa kwa Double Up Food Bucks au Produce Match.
4. Kutoa matunda na mboga zinazostahiki kwa bei isiyozidi bei inayotozwa wateja wasio wa DUFB au wasio wa mpango wa Produce Match.
5. Kutoruhusu kurejeshwa kwa matunda na mboga zilizonunuliwa kwa Double Up Food Bucks au Produce Match ili kubadilishanwa na pesa taslimu au kwa bidhaa zisizostahiki.
6. Kufuatiliwa na soko la wakulima au Hazina ya Soko la Wakulima ili kuhakikisha masharti ya mpango yanafuatwa.
7. Kutokomboa Double Up Food Bucksau Produce Match ili kutoa bidhaa zisizo za chakula.
8. Kutokubali Double Up Food Bucks au Produce Match zilizokwisha muda wake kutoka kwa wateja, ni sarafu ya sasa ya 2026 pekee itakayokubalika.
9. Kuwaelimisha wafanyakazi kuhusu miongozo ya mpango wa DUFB/Produce Match na matunda na mboga zinazostahiki.
10. Kuwasilisha Double Up Food Bucks na Produce Match ili kulipwa na soko la wakulima kwa mujibu wa miongozo ya soko. Siku ya mwisho ya kuwasilisha sarafu ya kurejeshewa pesa ni siku ya mwisho ya msimu wa 2026 wa soko hili.
11. Kubadilisha DUFB au Produce Match pekee ili kurejeshewa pesa kwenye soko ambako zilipokelewa.

Muuzaji na/au wafanyakazi wanaokiuka masharti yaliyo hapa juu wanaweza kuondolewa kwenye mpango na kutoruhusiwa kushiriki katika misimu ijayo.

Muuzaji, kwa kutia sahihi iliyo hapa chini, anahibitisha na kukubali miongozo na makubaliano yaliyoorodheshwa hapa juu.

MUUZAJI: ____________________________________

Jina (chapisha au uandike kwa herufi kubwa)

__________________________________

Saini (saini ya kielektroniki inakubaliwa)

__________________________

Tarehe